

CHUO CHA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI, MWEKA



TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Wananchi wote mnatangaziwa kwamba Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka kitaondosha kwa njia ya mnada wa hadhara magari matano (5) chakavu aina ya ISUZU Bus FSR 32F (1), Toyota Landcruiser Hardtop (3) na Toyota Land cruiser GX Station Wagon (1). Mnada huo utafanyika tarehe 15 Juni 2024 ndani ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka, kuanzia saa 4:00 asubuhi.

MASHARTI YA MNADA

1. Mnunuzi atalazimika kulipa papo kwa papo amana (Deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya chombo alichonunua na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa chombo husika na amana iliyolipwa haitarudishwa;
2. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua chombo alichonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo;
3. Gharama za kubadilisha umiliki ni jukumu la mnunuzi na atatakiwa kukamilisha taratibu za kumilikishwa chombo alichonunua kwa mujibu wa sheria ndani ya siku ishirini na moja (21);
4. Mtu yeote atakayetamka bei juu kisha akashindwa kulipa atachukuliwa kuwa ni mwenye kutaka kuvuruga mnada hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
5. Ruhusa ya kuangalia magari hayo itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya mnada husika.

Wananchi wote mnakaribishwa kushiriki katika mnada huu wa hadhara.

Imetolewa na:

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka,
214 Mweka Chini HM, 25216 Kibosho Mashariki
S. L. P. 3031,
Moshi, Kilimanjaro:
Simu Na. +255 692 883 333 / 766 883 333
Barua pepe: mweka@mwekawildlife.ac.tz
Totuti: www.mwekawildlife.ac.tz

*College of African Wildlife Management
Rector
Mweka, P. O. Box 3031, Moshi - Tanzania*